# KIFO
# NA
# KIYAMA

***"….walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika" Mwanzo 2:7***

***"Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa" Mwanzo 3:4***

***"Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima.Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi." Yohana 11:25***

# KIFO NA KIYAMA

**Toleo la kwanza; June 2012**

Kitabu hiki hakiuzwi. Kinatolewa BURE na KANISA LA MUNGU kwa madhumuni ya kuuelimisha uma wote uujue ukweli wa Biblia, ikiwa pia ni pamoja na kutii agizo la Bwana wetu Yesu Kristo lisemalo ***"mmepata bure, toeni bure" {soma Mathayo 10:8-9}.***

Kumbukeni tunafundisha kweli ya Biblia pekee na wala kamwe hatufundishi mafundisho ya madhehebu ya kidini au imani za watu fulani fulani tu kama ilivyozoeleka; hapa ni BIBLIA IMESEMA pekee.

Uchapaji wa kitabu hiki huwezeshwa na fungu la kumi *{yaani, zaka}* la waumini wa Kanisa hili la Mungu, pamoja na michango ya hiyari ya Wasomaji wetu.

Wewe pia waweza kushirikiana nasi kwa hiyari yako mwenyewe kuunga mkono kazi hii ya injili ya kweli kuenea zaidi kwa wengine kwa kutoa mchango wako ***{soma 2 Wakorintho 9:7-8}.***

**Haki zote zimehifadhiwa.**

## YALIYOMO; UK

UTANGULIZI……………………………………………………………………………………… 4
Sura ya kwanza…………………………………………………………………………...….5
KUUMBWA KWA MWANADAMU……………………………………………………...….5
Mwanadamu ni nini?.........................................................................................................................5
Je! uhai tulionao ni wa milele?..........................................................................................................6
Kifo ni nini?.......................................................................................................................................7
Ni nini husababisha kifo?..................................................................................................................7
Udanganyifu wa Shetani…………………………………………………………………….9
Udanganyifu wa kidini……………………………………………………………………….9
Sura ya pili………………………………………………………………………...……..11
SHETANI HUJIGEUZA……………………………………………………………………..11
Ibada za wafu……………………………………………………………………………..…12
Mila na desturi potofu…………………………………………………………………….…..13
Sura ya tatu…………………………………………………………………………………14
KIYAMA YA WAFU {UFUFUO}……………………………………………………...…14
Vipindi tofauti vya ufufuo……………………………………………………………………15
Ufufuo wa kwanza………………………………………………………………………..…16
Ufufuo wa pili………………………………………………………………………....…17
Ufufuo wa tatu……………………………………………………………………………..19
Sura ya nne…………………………………………………………………………………20
NI NINI HATIMA YA WOTE WANAOKATAA KUTUBU?...........................................................20
Je! kulia unapofiwa ni dhambi?.......................................................................................................21
Hitimisho………………………………………………………………………………...…22

# UTANGULIZI

Kati ya mambo ambayo yanasumbua akili za Wanadamu na kutufanya kujiuliza maswali mengi ambayo majibu yake yako nje ya ufahamu wetu ni pamoja na suala zima la kifo *{au mauti}*. Tangu mwanzo tumesikia na pia tunaendelea kushuhudia leo vifo vingi vinavyosababishwa na mambo mbali mbali. Tena kibaya zaidi ni kwamba kila uchao idadi ya vifo pia huongezeka zaidi.

Magonjwa mbali mbali yanasababisha vifo vya maelfu ya watu kila leo. Uhai wa wanadamu unatishiwa kuangamizwa na Ukimwi, Ebola, Malaria, Kansa n.k. Haya yote hupeleekea kifo ambacho huibua maswali mengi yasiyo na ufumbuzi kwa ufahamu wa kibinadamu. Lakini je! ni nini chanzo cha magonjwa haya yote na hatimaye kifo?

Vita vilivyozagaa karibia kila kona ya Dunia vinasababisha vifo vya maelfu ya watu kila siku. Kutokana na vita hivyo; watu wengi wamekimbia nchi zao wakijaribu kuokoa maisha yao. Lakini inaumiza zaidi kuona watu waliokimbia kifo katika nchi zao wakiangamia pamoja, tena kwa wingi baharini na kufa maji baada ya vyombo vya usafiri wanavyotumia kushindwa kuhimili idadi ya abiria na misukosuko ya bahari na hivyo kuzama na kusababisha vifo vya kutisha vya maelfu ya watu. Kadhalia wale wanaofaulu kuvuka salama pia bado wengine miongoni mwao wanakufa kwa njaa, baridi na magonjwa ya milipuko katika makambi maalumu wanapohifadhiwa katika nchi za ugenini.Wengine pia uuawa na askari wa usalama kwa madai ya kwamba watu hao ni wavamizi na wahamiaji haramu wanaovunja sheria za nchi hizo. Katika kila hatua ni VIFO, VIFO, VIFO! Ni nini chanzo cha vifo hivi, na ni nini ufumbuzi wa tatizo hili sugu linalozidi kumea kwa kasi zaidi?

Hata hivyo, si mambo haya tu ambayo ndiyo husababisha vifo. Utakumbuka ni watu wangapi ambao hupoteza maisha yao kila siku na kila mwaka kwa majanga ya dunia kama vile ukame ambao husababisha njaa, na kisha njaa kusababisha vifo. Bila kusahau mafuriko, maporomoko ya ardhi, matetemeko ya nchi, vimbunga, sunami n.k. Vyote hivi vinawinda uhai wa mwanadamu ili vimsababishie kifo ambacho pia mwanadamu huyo anakiogopa sana, maana hana uwezo wa kujikinga nacho!

Mambo haya pamoja na mengine kadha wa kadha yamewafanya wanadamu kujiuliza maswali mengi ya msingi japokuwa mpaka leo hawajapata majibu sahihi ya maswali yao. Tunajiuliza; kifo ni nini? Ni nini/nani husababisha kifo? Kwa nini watu wanakufa? Je! wafu wana hali gani? Wako wapi, na wanafanya nini huko waliko? Je! tutaendelea kufa mpaka lini? Na je! kuna maisha baada ya kufa? Pamoja na maswali mengine mengi kama haya!

Mpendwa msomaji wa kitabu hiki; tunaamini wewe pia ni miongoni mwa wale wenye kujiuliza maswali haya na mengine mengi zaidi kuhusu kifo. Lakini ukweli ni kwamba; hakuna mwanadamu awaye yote awezaye kuyajibu maswali haya kwa usahihi. Sasa je! tufanyeje? Tubaki na maswali yetu hivyo hivyo bila majibu? La hasha! Kuna habari njema kwetu, kwamba; ***"yuko Mungu mbinguni afunuaye siri" {soma Danieli 2:28}.*** Na kupitia kwa Maandiko yake Matakatifu, yaani Biblia; basi Mungu yuko hapa hivi sasa akitufunulia siri hii kwa majibu sahihi ya maswali yetu tuliyoshindwa kuyajibu sisi wenyewe. Sasa je! uko tayari kumsikiliza Mungu aliyetuumba na ambaye ndiye chanzo cha maisha na mwenye ufahamu wa mambo yote? Maana yeye anasema; ***"Mimi ni BWANA, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida, nikuongozaye kwa njia ikupasayo***

***kuifuata" Isaya 48:17.*** Sasa basi; hebu na tusikilize kile anachotuambia ili tupate majibu sahihi ya maswali yetu yote yahusuyo kifo na kiyama *{ufufuo}* ya wafu. Fuatana naye sasa.

### Sura ya kwanza

# KUUMBWA KWA MWANADAMU

## Mwanadamu ni nini?

Ili tuweze kuelewa vyema kwamba kifo ni nini na nini chanzo chake; basi tunapaswa kwanza kumuuliza Mungu muumba wetu kwamba, "sisi wanadamu ni nini ama ni kitu gani hasa?

Kabla Mungu hajamuumba mwanadamu, alikusudia kumuumba kwa namna hii kwamba; ***"Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu…" {Mwanzo 1:26},*** kwa madhumuni ya kuitawala dunia kama sehemu ya ufalme wa mbinguni baada ya uasi wa malaika *{kwa maelezo zaidi kuhusu hili, agiza ujumbe wetu usemao* ***"MWANADAMU NI NANI?".*** *ama ule usemao* ***"UFALME WA MBINGUNI",*** *ili ujifunze zaidi, na utatumiwa bure ujumbe huo}.* Na ili mwanadamu awe kama Mungu; uumbwaji wake ulikuwa uchukue hatua kuu tatu na ndipo awe kama Mungu na kisha aitawale dunia kama Mungu alivyokusudia.

Hatua ya kwanza ya uumbwaji wa mwanadamu ilikuwa kama ifuatavyo; ***"BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai" Mwanzo 2:7.*** Naam, wapendwa; Muumba wetu ametuambia kwamba sisi ni mavumbi ya ardhi *{yaani udongo},* na pumzi yake aliyotupulizia puani ndiyo itufanyayo kuwa hai. Kwa maana kwamba; katika hatua hii ya kwanza, bado hatujawa kama Mungu; yaani bado hatujaumbwa kwa sura ya Mungu; maana anasema, ***"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba" Mwanzo 1:27.***

Je! tunamaanisha nini hapa? Ni kwamba, tunapozungumzia kuumbwa kwa mfano wa Mungu, ina maana kwamba maumbile *{mwonekano/taswira}* yetu yako sawa na yale ya Mungu. Kama tulivyo na viungo mbali mbali vya mwili kama vile kichwa, macho, kinywa, mikono, miguu, kifua, tumbo n.k. ndivyo alivyo pia Muumba wetu ***{soma Danieli 7:13; Ufunuo 1:13-15; 14:14}.***

Na tunapozungumzia kuumbwa kwa sura ya Mungu; ina maana ya kuumbika tabia ya Mungu ndani yetu ***{soma Waefeso 4:24},*** hali ambayo sisi hatukuumbika kwayo; maana hiyo ni hatua ya pili hali sisi tungali katika hatua ya kwanza. Na tusisahau ya kuwa ***"Mungu ni Roho",*** bali sisi ni ***"mavumbi ya ardhi",*** ambao uhai wetu unategemea pumzi ya Mungu ***{soma Yohana 4:24; Mwanzo 2:7.***

Wapendwa; hii ina maana kwamba; uhai tulionao ni sawa sawa na uhai walionao wanyama; yaani kile kinachotufanya kuwa hai, ndicho kile ambacho pia kinawafanya wanyama kuwa hai ***{soma Mwanzo 7:21-23}***. Ni kwa nini tunalifafanua jambo hili kwa mapana kiasi hiki? Naam; tukijielewa *{tukijifahamu/tukijitambua}* vyema kwamba sisi ni nini hasa; basi hili litatusaidia pia kuelewa vyema kwamba kifo ni nini hasa. Kwa hivyo basi tumeona kwamba, sisi ni mavumbi ya ardhi *{yaani*

*udongo}*, na uhai wetu ni pumzi ya Mungu iliyo katika pua zetu na wala si kitu kingine. Na kwa hivyo basi; hatuko sawa na Mungu, maana pia tumeona kwamba Yeye ni Roho, na huku sisi ni mavumbi, na pia hatujaumbwa kwa sura *{yaani tabia}* yake mpaka sasa.

## Je! uhai tulionao ni wa milele?

Wapendwa wetu; je! hii **"pumzi ya uhai"** tuliyopuliziwa puani tukawa nafsi hai, ambayo pia tumeona ikiitwa **"pumzi ya roho ya uhai"** ***{rejea Mwanzo 7:22}*** ni yenye kudumu milele? Je! ni kitu ambacho mwanadamu akiisha kupuliziwa kinadumu milele na wala hakiwezi kutoweka na kupotea kabisa? Muumba wetu anatuambia kwamba; ***"Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke Siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa taabu. Yeye huchanua kama vile ua, kisha hukatwa; Hukimbia kama kivuli, wala hakai kamwe" Ayubu 14:1-2; soma pia Isaya 40:6-8.*** Tena; ***"Lakini mwanadamu hufa, huifariki dunia; Naam, mwanadamu hutoa roho, naye yuko wapi?" Ayubu 14:10.***

Mungu wetu anatuambia kwamba, huu uhai *{roho}* aliotupa ni wa kitambo kidogo tu na wala si wa kudumu *{si wa milele}*. Na ili tumwelewe vyema; ametutolea mfano wa ua. Sote tunafahamu jinsi ambavyo ua linapochanua hupendeza sana macho kwa urembo wake kiasi cha kutamani kulitazama likiwa vivyo hivyo siku zote. Lakini pia kama tujuavyo kwamba, baada ya muda mchache tu, ua huanza kunyauka na kupoteza urembo wake na hatimaye kuharibika kabisa na kupoteza thamani yake kabisa. Naam; hivi ndivyo uhai *{roho}* wetu ulivyo. Ni uhai wa kitambo kidogo tu, na baadaye hutoweka kabisa. Kama vile ua lichanuapo linavyokuwa na thamani, kadhalika mwanadamu anapozaliwa huwa na thamani pia. Na kama vile thamani ya ua ilivyo wakati wa urembo wake, kadhalika thamani ya mwanadamu wakati wa uhai wake. Tena kama vile thamani ya ua ipoteavyo mara baada ya kunyauka, kadhalika thamani ya mwanadamu hupotea kabisa mara baada tu ya pumzi *{roho}* yake kutoweka. Na tena kama vile ua likiishanyauka huitwa uchafu/takataka; kadhalika mwanadamu akiishapoteza uhai wake huitwa maiti, marehemu, wengine huita kitundu n.k. Na japo tunajifariji kwa majina hayo kana kwamba bado mfu ana thamani kidogo, lakini ukweli ni kwamba; kama mnyama anavyokufa na tunamwita mzoga, ndivyo mwanadamu alivyo mzoga pia baada ya pumzi yake kutoweka. Kumwita mwanadamu aliyetokwa na uhai wake eti **"mwili wa marehemu"** hakuna tofauti na kumwita **"mzoga".**

Wapendwa; japokuwa ukweli huo unaweza kuwaudhi wengine, lakini lazima uwekwe wazi mbele yetu ili anayetaka kujitambua/kujifahamu ya kuwa yeye ni nini hasa, basi na atambue; na yule asiyetaka pia apuuze, japo ukweli utabaki kuwa pale pale tu. Ama je! haya tuyasemayo ni mawazo na dhana zetu wenyewe? Je! ni mambo ya kutungwa na kupotosha tu? La, hasha! Ni Muumba wetu ndiye anayetuambia hivi. Naam; kupitia kwa Sulemani, Mungu anasema; ***"Nikasema moyoni mwangu, Ni kwa sababu ya wanadamu, ili Mungu awajaribu, nao waone ya kuwa wao wenyewe wafanana na wanyama. Kwa maana linalowatukia wanadamu linawatukia wanyama; jambo moja lawatukia; anavyokufa huyu ndivyo anavyokufa huyu; naam, wote wanayo pumzi*** *{roho}* ***moja; wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama; kwa maana yote ni ubatili. Wote huenda mahali pamoja; wote hutoka katika mavumbi; na hata mavumbini hurudi tena" Mhubiri 3:18-20.*** Naam; mwenye masikio na asikie.

## Kifo ni nini?

Je! kifo ni nini? Ni nini hutokea/hufanyika ndipo mtu awe amekufa? Tumeeleza vyema kuwa mwanadamu ni nini hasa. Biblia imetuambia kuwa mwanadamu ni mavumbi ya ardhi, ameumbwa kwa udongo. Na kwamba kile kinachoufanya udongo huo kuwa hai ni pumzi ya Mungu iliyowekwa puani mwake. Kwa maana kwamba, muunganiko wa udongo huo ulioumbwa kwa mfano *{kwa maumbile/taswira}* wa Mungu, pamoja na pumzi ya Mungu ndivyo vinavyomfanya *{vinavyomtengeneza}* mwanadamu. Sasa je! kufa kuna maana gani? Ama je! kifo ni nini?

Naam, wapendwa; kuunganishwa kwa udongo *{mwili}*na pumzi ndiko kunamfanya mtu aliye hai. Kadhali kutenganishwa kwa udongo *{mwili}* na pumzi ndiko kunakoitwa kufa. Kwa maana kwamba; kutengana kwa mwili na pumzi ya uhai *{roho},* kitendo hiki ndicho kiitwacho kifo. Hebu na tulithibitishe jambo hili kwa maandiko tafadhali. Naam; Maandiko yanauliza; ***"Lakini mwanadamu hufa, huifariki dunia; Naam; mwanadamu hutoa roho, naye yuko wapi? Ayubu 14:10.*** Maandiko yanajibu yakisema; ***"Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, Siku hiyo mawazo yake yapotea" Zaburi 146:4.*** Tena yanasema; ***"Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, Nayo roho {pumzi ya uhai} kumrudia Mungu aliyeitoa" Mhubiri 12:7.***

Maandiko yameeleza wazi kwamba; kifo ni kitendo cha udongo *{mwili}* kutengana na pumzi *{roho}.* Na vitu hivi viwili vinapotengana, kila kimoja kinarudi mahali pale kilipokuwapo awali. Kwa maana kwamba; pumzi *{roho}* ya uhai inaondolewa na Mungu aliyeiweka, na kisha mavumbi *{mwili}* yanarudi mavumbini yalikokuwako awali. Kwa lugha rahisi ni kwamba; baada ya kutengana kwa mavumbi *{mwili}* na pumzi *{roho},* basi hapo mwanadamu hayupo tena, ametoweka kabisa kama vile ua litowekavyo na lisiwepo tena. Naam; hii ndiyo maana halisi ya kifo kwa mujibu *{kwa maelezo}* wa Maandiko Matakatifu ya Muumba wetu. Mwenye masikio na asikie.

## Ni nini husababisha kifo?

Je! ni nini husababisha kifo? Ama je! ni nani husababisha kifo? Naam; ni nani awauaye wanadamu? Je! ni Mungu ama ni Shetani? Naam; ni nini hasa ambacho huleta kifo?

Wapendwa; Biblia inaelezea kitendo cha kufa ama swala la kifo *{mauti}* kama matokeo ya dhambi. Kwa maana kwamba, atendaye dhambi ndiye afaye, na pasipo dhambi hakuna kifo. Imeandikwa; ***"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" Warumi 6:23.*** Lakini je! dhambi ni nini? Naam; dhambi ni kitu gani hasa ambacho mtu akifanya kinamsababishia kifo? Biblia inajibu kwamba; ***"Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi" 1 Yohana 3:4.*** Kitendo cha kuasi sheria za Mungu ndicho kiitwacho dhambi, na ndiyo isababishayo ama iletayo kifo *{mauti}; soma pia* **Yeremia 2:19.**

Sasa je! ni kusema kwamba Adamu na Hawa mkewe walitenda dhambi? Je! waliasi sheria za Mungu na hivyo kitendo hicho kikawaletea kifo? Naam; baada ya Mungu kuwaumba wanadamu wa kwanza *{yaani Adamu na Hawa}* katika hatua ya kwanza ya uumbwaji wao *{yaani , katika hatua ya mwili huu wa damu na nyama}* na kuwaweka katika bustani ya Edeni; aliwaagiza akisema; ***"Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika" Mwanzo 2:16-17.***

Naam; baada ya maagizo *{sheria}* hayo ya Mungu kwa mwanadamu; je! mwanadamu aliitii sheria hiyo ama aliiasi? Biblia inajibu ikisema; ***"Basi nyoka {yaani Shetani; soma Ufunuo 12:7-9} alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya. Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala" Mwanzo 3:1-6.*** Kwa hivyo, iko wazi kwamba Adamu na mkewe waliasi sheria ya Mungu, na hivyo uasi huo ukawaletea mauti *{kifo}.*

Kumbukeni; tuliona awali kwamba Mungu alikusudia kumuumba mwanadamu ili ampe utawala wa dunia. Na pia kwamba ili mwanadamu aitawale dunia, ni lazima aumbike na kuwa kama Mungu alivyo. Tena tukaona ya kuwa, uumbwaji wa mwanadamu mpaka afikie ukamilifu wa uungu unachukua hatua kuu tatu. Hatua ya kwanza ni kuumbwa katika mwili huu wa damu na nyama tulionao. Hatua ya pili ni kujenga ufahamu wa Mungu akilini ambako ndiko kuumbwa kwa sura *{tabia}* ya Mungu. Na hatua ya tatu na ya mwisho ni kubadilishwa na kufanywa viumbe wa kiroho. Na hivyo basi; mwanadamu alipoumbwa katika hatua hii ya kwanza, hakuwa mtakatifu wala hakuwa mwovu. Baada ya kuumbwa katika hatua ya kwanza ya ambayo ni ya mwili huu wa damu na nyama, Mungu alimwekea aina mbili za maisha mbele yake ili achague aina mojawapo atakayoishi kwayo. Kwa kuchagua kutii sheria ya Mungu *{yaani kutokula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya, na badala yake ale matunda ya mti wa uzima}* angekuwa amechagua maisha ya Mungu ya milele yasio na kifo. Na hivyo angejifunza maisha ya Mungu ambayo ni hatua ya pili ya uumbwaji na baada ya kufaulu angebadilishwa na kuwa kiumbe wa kiroho kama vile Mungu alivyo.

Lakini pia kwa kuasi sheria ya Mungu *{yaani, kula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya},* alichagua maisha ya Shetani yaletayo uharibifu na mwishowe mauti kama ilivyo leo hii. Na hivyo basi; badala ya kuumbika tabia *{sura}* ya Mungu, mwanadamu aliumbika tabia *{sura}* ya Shetani; na hivyo Mungu akasitisha uumbwaji wa mwanadamu angali katika hatua hiyo ya kwanza. *{Kwa maelezo ya kina zaidi kuhusu miti hii miwili inayowakilisha aina {mifumo/namna} mbili za maisha; basi agiza ujumbe wetu usemao,* ***"MITI MIWILI",*** *ili ujifunze zaidi, na ujumbe huo utatumiwa bure}.*

Sasa basi; ikiwa Adamu na mkewe ndio waliotenda dhambi, mbona sasa watu wote wanakufa? Biblia inajibu ikisema; ***"Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja {yaani, Adamu} dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi" Warumi 5:12, soma pia 3:10-18.*** Kwa hivyo basi; ni dhambi *{yaani, uasi wa sheria za Mungu na kufuata maisha ya udanganyifu ya Shetani}* ndiyo isababishayo ama iletayo mauti *{kifo}* na wala si kitu kingine ***{soma Yohana 8:44}.*** Na tena, sote tumetenda dhambi, na matokeo *{malipo}* yake ni mauti.

## Udanganyifu wa Shetani

Kama tulivyoona, wazazi wetu wa kwanza *{yaani, Adamu na Hawa}* walivyodanganywa na Shetani *{nyoka}* na kuchagua kuyafuata maisha yake bandia ya uharibifu na hatimaye kifo; basi tangu hapo, wao na uzao wao *{yaani, ulimwengu wote}* hadi leo hawakujifahamu/hawajifahamu kuwa wao ni nini hasa, na wakabakia tu na ufahamu huo wa udanganyifu waliojifunza kutoka kwa Shetani ya kuwa wao ni sawa na Mungu. Naam; mpaka leo hii, mwanadamu anafahamu ya kuwa yeye ni kiumbe asiyekufa na aliye sawa na Mungu; yaani mwenye ufahamu wa kumwezesha kuishi mwenyewe hata pasipo uwepo wa Mungu. Maana Shetani alimdanganya mwanadamu ya kuwa, ***"Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku utakayokula matunda ya mti huo*** *{waliokatazwa na Mungu wasile},* ***mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya" Mwanzo 3:4-5.***

Ukiangalia katika jamii yote leo duniani, utaona kila mmoja akifanya jitihada za kuonekana mkuu na wa maana sana zaidi yaw engine, na kufanya bidii ya kujilimbikizia wingi wa mali ili kuonesha uwezo wake na kutaka kuheshimiwa na watu wote. Na wakitaka kufikia katika kiwango hicho, basi hulazimika kutumia njia yo yote ile hata kama ni mbaya *{haramu}* kiasi gani, ilimradi tu wapate heshima na kukubalika kwa watu. Udanganyifu wa Shetani umempofusha mwanadamu fikira hata asitambue kwamba yeye hana heshima yo yote, maana hana tofauti na mnyama ***{soma Mhubiri 3:18-20}.*** Hali hii imewafanya wasikubali kudharauliwa hata kama ni wanyonge na kujaribu kujihami *{kujitetea}* na kuonesha kuwa wao si duni kwa njia yo yote ile. Lakini ukweli unabaki kuwa kwamba, huku kujisifu, kujigamba na kujiona wakuu kama Mungu, ni kujidanganya tu. Tena huku kujidhania kuwa tu viumbe wenye roho isiyokufa, ni ubatili mtupu, ni kama kufukuza upepo.

Mungu wetu ametueleza ya kwamba sisi ni mavumbi ya ardhi *{udongo},* na pumzi yake ndiyo itupayo uhai ***{soma Mwanzo 2:7};*** na mara tu aitoapo pumzi hiyo katika pua zetu, basi tunakufa na kuurudia udongo ambao kwa huo tuliumbwa ***{soma Zaburi 146:4; Mhubiri 12:7}.*** Naam; baada ya hapo, tunatoweka kama maua, na wala hatupo tena mahali po pote pale ***{soma Ayubu 14:1-2; Isaya 40:6-8}.*** *{kwa msaada zaidi juu ya jambo hili, basi agiza ujumbe wetu usemao,* ***"THAMANI YA UKRISTO",*** *ili ujifunze zaidi, na ujumbe huo utatumiwa bure}.*

## Udanganyifu wa kidini

Kutokana na udanganyifu wa Shetani tangu pale bustanini Edeni, basi wanadamu wameendelea kuutumia uongo huo kama ufahamu *{ujuzi}* wao wa maisha mpaka leo hii. Hata wengi wa wale wanaodai kumwamini, kumwabudu na kumtumikia Mungu, nao pia wanaendelea kuishi kwa ufahamu huo wa Shetani na hivyo hawajitambui mpaka sasa. Kwa kuendelea kuishi kwa udanganyifu huo wa Shetani; basi utawasikia wahubiri wengi sana wakiwafundisha watu ya kuwa, mtu anapokufa akiwa mwenye dhambi, basi roho *{pumzi}* yake hupelekwa motoni mahali panapoitwa Jehanamu ili akateswe huko kwa kuungua katika moto huo kwa maumivu makali ya milele! Tena ya kwamba, endapo mtu akifa akiwa mwenye haki, basi huyo naye roho *{pumzi}* yake hupelekwa mbinguni kwa Mungu, mahali panapoitwa Paradiso, na kwamba huko anaburudishwa kwa vyakula na vinywaji vitamu huku akifanya kazi ya kumwimbia, kumsifu na kumwabudu Mungu huko mbinguni milele na milele! Huu wote ni ule udanganyifu wa Shetani unaendelea kutumiwa hata na viongozi wa kidini, maana wameshindwa kupambanua sauti ya Mungu wao na sauti ya Shetani; na hivyo wao pasipokujua, wanamtumikia Shetani huku wakidhani ya kwamba wanamtumikia Mungu wa mbinguni! Hebu na tuyadhibitishe haya kwa Maandiko tafadhali.

Wapendwa; tumeeleza kwa mujibu wa Maandiko jinsi ambavyo mwanadamu hufa. Kwamba kifo ni kitendo cha pumzi *{roho}* ya Mungu kuondolewa puani mwa mwanadamu na hivyo mwili *{udongo}* kuharibika kwa kukosa huo uhai na kurudi kuwa udongo kama hapo awali. Baada ya hapo, basi mwanadamu hayupo tena, ametoweka kabisa. Na kwa sababu hiyo basi; Mungu anatuambia, ***"Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako; Kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe" Mhubiri 9:10.*** Je! haya ni maneno yetu wenyewe? La, hasha! Ni Mungu amesema. Uwe mwema ama mwovu, baada ya kufa umetoweka kabisa, hakuna kinachoendelea kwako. Mwema na mwovu, wote wako kuzimu. Lakini je! Kuzimu ni wapi? Neno kuzimu lina maana ya kutokuwepo mahali po pote pale, kwamba ni duniani ama mbinguni, ni hali ya utupu, na si mahali fulani ambako maisha yanaendelea kwa namna nyingine baada ya kufa. Naam; elewa na fahamu jambo hili tafadhali. Kwamba kauli ya Muumbaji wetu ni kuwa, mwanadamu hufa na kutoweka kabisa na asiwepo tena ***{soma Mwanzo 2:17}.*** Lakini pia kauli ya Shetani ni kwamba, mwanadamu hafi, ana roho {pumzi} isiyoweza kutoweka milele kama ya Mungu ***{soma Mwanzo 3:4-5}.*** Kwa hivyo basi; ni juu yako kuchagua mwenyewe kwamba ni nani utakayemwamini; utamwamini Mungu kwamba mwanadamu hufa na kutoweka kabisa, ama utamwamini Shetani kwamba mwanadamu hafi, ni wa milele; uamuzi ni wako!

Wapendwa; Maandiko Matakatifu ya Mungu ambayo ni sauti yake kwetu, yanaendelea kututhibitishia ukweli huu yakisema; ***"Kwa sababu walio hai*** *{wema na waovu}* ***wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu*** *{wema na waovu}* ***hawajui neno lo lote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote lifanyikalo chini ya jua" Mhubiri 9:5-6.*** Hili nalo ni Mungu ndiye atuambiaye. Je! utamwamini? Tena kwa wale waliodanganywa na Shetani ya kwamba, wenye haki wanapokufa roho *{pumzi}* zao zinaenda kuishi pamoja na Mungu mbinguni, huku roho *{pumzi}* za waovu zikipelekwa motoni kuteswa; basi Mungu mwenyewe anasema; ***"Sio wafu wamsifuo Bwana, wala wo wote washukao kwenye kimya".*** Kwa nini? ***"Maana mautini hapana kumbukumbu lako; Katika kuzimu ni nani atakayekushukuru?" Zaburi 115:17; 6:5.***

Baada ya muda mrefu kupita; tena baada ya kuwa watu wengi wamekufa, wema kwa waovu; Yesu Kristo alikuja duniani akitokea mbinguni, na akatuambia hali halisi ya huko mbinguni akisema; ***"Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni*** *{akiwa hai ama baada ya kufa}*, ***ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Adamu" Yohana 3:13.*** Na hata mitume wake pia walifahamu na kuamini vivyo hivyo; naye Petro akasema; ***"Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki*** *{alikufa}* ***akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo…Maana Daudi hakupanda*** *{hakwenda}* ***mbinguni…" Matendo 2:29,34.*** Sasa rafiki; je! watakatifu ni akina nani kama si hao akina Daudi ambao maandiko yanasema wazi kwamba hawakwenda mbinguni? Mwenye masikio na asikie!

## Sura ya pili

# SHETANI HUJIGEUZA

Watu wengi wamekwisha kutokewa na ndugu, jamaa na hata marafiki zao waliokwisha kufa. Na hii ni kwa njia mbali mbali kwa mfano; wengine kwa njia ya wazi wazi, wengine katika ndoto, na wengine kwa waganga wa jadi wenye pepo wa utambuzi, maarufu kama waaguzi. Lakini je! hawa ni wafu hao halisi ama ni akina nani hawa? Maana hii imechangia kwa sehemu kubwa kuwafanya watu kuamini kuwa wafu wanaendelea kuishi kwa namna fulani mahali fulani. Ni akina nani hawa wanaojitokeza kwa watu? Je! ni wao wafu halisi? Hebu jitahidi usome kitabu cha ***1 Samweli 28*** sura yote upate habari kamili ya kisa tunachokwenda kukigusia kidogo tu hapa. Hapa tutachambua baadhi ya mafungu tu.

Wana wa Israeli walielewa vema ukweli kuhusu wafu; kwa maana kwamba, walijua yote sawa sawa na yale yote tuliyokwisha kujifunza hapo nyuma. Na katika nchi hiyo ya Israeli hakuruhusiwa mtu ye yote kuishi ikiwa ana imani tofauti na hiyo ya hao Waisraeli. Na watu kama hao walifukuzwa nchini humo ili wasije wakawafanya watu kuamini mambo mageni tofauti na yale waliyofundiswa na Mungu wao, ambaye ni wetu pia. Katika kitabu cha ***1 Samweli 28:3*** biblia inasema hivi**; *"Basi Samweli*{*nabii*}*alikuwa amefariki dunia, nao Israeli wote walikuwa wamemwomboleza, na kumzika huko Rama, ndani ya mji wake mwenyewe. Tena Sauli*** {*mfalme wa Israeli*} ***alikuwa amewaondolea mbali hao wenye pepo wa utambuzi na wachawi katika nchi***". Katika fungu hili tutoke na mambo makuu mawili; jambo la kwanza; Samweli nabii alikuwa amekwisha kufa na kuzikwa huko nyumbani kwake Rama. Na jambo la pili; Wachawi na watambuzi wenye pepo *{waganga wa jadi}* walikuwa wamefukuzwa nchini, kwa maana wao wana miungu yao tofauti na MUNGU wa Israeli. Tafadhali soma kisa chote ili uelewe zaidi. Sauli kwa kuwa Mungu wa Israeli amemkataa *{kwa kutokutii kwake}* na wala hamjibu maswali yake; aliamua kuwaendea huko wanakoishi hao wachawi na wenye pepo wa utambuzi aliokuwa amewafukuza yeye mwenyewe. Na kwa sababu alijua kwamba lile analolitenda ni kosa *{dhambi},* alikwenda usiku ili watu wasimuone asije akapigwa kwa mawe. Basi Sauli baada ya kujadiliana mengi na mmoja wa hao wenye pepo, basi shida yake ikaanza kushughulikiwa. Katika sura hiyo hiyo ya ***1 Samweli 28:12-14*** biblia inasema hivi*; **"Hata yule mwanamke*** {*mchawi/muaguzi*} ***alipomuona Samweli alilia kwa sauti kuu; na yule mwanamke akamwambia Sauli, akasema, Mbona umenidanganya? kwa kuwa wewe ndiwe Sauli. Mfalme akamwambia Usiogope; waona nini? Yule mwanamke akamwambia Sauli, Naona Mungu anatoka katika nchi. Naye akamuliza, Ni mfano wa nini? Akajibu, Ni mzee anazuka, naye amefunikwa vazi. Basi Sauli akatambua ya kwamba ndiye Samweli mwenyewe, akainama uso wake mpaka nchi, akasujudu."***

Wapendwa; utagundua kwamba, dhambi moja huzaa nyingine, maana hata wakati Samweli alipokuwa angali hai Sauli hakumsujudia kulingana na amri za Mungu ambazo zilikuwa ndiyo mwongozo wa nchi yao {***soma Kutoka 20:4-6}.*** Lakini sasa anamsujudia; na utagundua kuwa huyu anayesujudiwa si Samweli halisi bali ni shetani! Ndugu zangu, Shetani ni mjanja sana, maana katika mstari wa ***15-19*** ni majadiliano kati yake na Sauli. Na kwa sababu ametokea katika sura ya Samweli; akaamua kutumia maneno yale yale aliyoyasema Samweli wakati wa uhai wake. Hebu linganisha ***1 Samweli 28:15-19 na 1 Samweli 15:28.*** Maana tumekwisha kuona kuwa waliokwisha kufa hawajui neno lo lote lile; na mwanzoni katika ***1 Samweli 28:3*** biblia imetukumbusha kuwa Samweli akikuwa amekwisha kufa na kuzikwa huko nyumbani kwake Rama. Na ikiwa wafu hawajui neno lo lote lile;

sasa je! huyu Samweli anayezungumza hapa na Sauli ni nani? Maana Ayubu pia anatuambia kuwa mtu akiisha kufa***; "Wanawe hufikilia heshima, wala yeye hajui;Kisha wao huaibishwa, lakini yeye hana habari zao." Ayubu 14:21*** Sasa mbona huyu Samweli yeye anajua habari ya Waisraeli kuhusu vita vyao na Wafilisti? Je! huyu ni Samweli kweli? Hebu sasa na tupate jibu la hakika katika ***2 Wakorintho11:14-15,*** nalo linasema; ***"Wala si ajabu.Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki,ambao mwisho wao utakuwa sawa sawa na kazi zao****."* Mungu atukuzwe; maana kumbe huyo ni Shetani anayejigeuza awe mfano wa Samweli! Kwa hivyo, wale wote waliokwisha kutokewa na ndugu, jamaa, rafiki au mtu ye yote yule ambaye alikwisha kufa; tangu leo mtambue kuwa hao mliowaona si wao halisi, bali ni Shetani anayejigeuza awe mfano wao; maana wafu hawajui lo lote wala hawapo po pote pale. Tena mwisho wa huyo Shetani pamoja na hao wamwaminio utakuwa sawa sawa na kazi zao; kwa maana kwamba, wataangamia wote pamoja milele. Sasa ikiwa umewahi kutokewa na mmoja wapo wa waliokufa; kwamba ni baba, mama, mtoto, mke, mume, babu, bibi au ye yote yule; basi jua kwamba si wao, bali ni Shetani anayejigeuza awe mfano wao. Na ikiwa anaendelea kukutokea, kwa imani mkemee katika Jina la Yesu Kristo, na wala hatakutokea tena kamwe. **Mwenye masikio na asikie; ni Biblia yasema.**

## Ibada za wafu

Kutokana na kuamini kuwa wafu wako hai na wanaendelea kuishi mahali fulani; watu wengi wamekuwa wakiwafanyia ibada kwa njia mbalimbali. Kwa mfano; wengine kabla ya kuanza kula, humega sehemu ndogo ya chakula hicho na kukiweka chini kwa madai kwamba hao wafu waliowapa jina la ***"Wazee wetu"*** wanapaswa kula kwanza ili wakibariki chakula hicho. Na ibada hizi hutofautiana kwa kila tabaka na jamii fulani za watu. Kwa hivyo sitaweza kueleza moja baada ya nyingine maana ni nyingi sana na hata mimi mwenyewe nyingine nyingi pia sizielewi. Bila shaka wewe pia unajua jamii au kabila lako wanavyofanya; na hata jamii nyinginezo zinazowazunguka pale unapoishi, na hata kwingineko kote ulikowahi kufika ama kusikia. Na ibada hizi hutegemea hali zote mbili za maisha ya wanadamu; nikimaanisha katika hali ya shida na raha. Kwa mfano; katika raha hufanyika wakati wa harusi, jando, wakati wa mavuno, ushindi vitani na mengine mengi kama hayo. Vilevile katika shida hufanyika wakati wa mafuriko, ukame, njaa, vimbunga, magonjwa ya milipuko, vifo vya kawaida, kushindwa vitani na mengine mengi kama hayo. Kile tunachokizungumzia hapa ni ibada za wafu kwa ujumla wake. Na watu hao wafanyao hizo ibada mara nyingi hujibiwa maombi yao; sasa je! ni hao wafu halisi wanaoyajibu maombi hayo? La, hasha; bali ni yule Shetani ajigeuzaye ndiye anayewajibu, maana ndiye wamwabuduye huku wakidhani kuwa wanawapa heshima wafu wao*{wazee wao}*. Ibada za namna hii kwa ujumla wake pasipo kutofautisha kuwa jamii fulani na fulani wanafanyaje; je! Biblia inakubaliana nazo? Ni nini anachosema Mungu juu ya mambo haya? Katika kitabu cha kumbukumbu la torati biblia inatuambia hivi; ***"Asionekane kwako mtu ampitishaye mwanawe au binti yake kati ya moto, wala asionekane mtu atazamaye bao, wala mtu atazamaye nyakati mbaya, wala mwenye kubashiri, wala msihiri, wala mtu alogaye kwa kupiga mafundo, wala mtu apandishaye pepo, wala mchawi, wala mtu awaombaye wafu." Torati 18:10-11*** Na tena ***"Msichanje chale yo yote katika nyama ya miili yenu kwa ajili ya wafu, wala msiandike alama miilini mwenu;mimi ndimi Bwana." Walawi 19:28*** Tena; ***"Ninyi mmekuwa wana wa Bwana, Mungu wenu;msijitoje miili yenu, wala msifanye upaa katikati ya macho yenu kwa ajili ya aliyekufa." Torati 14:1*** Kwa hivyo aina yo yote ile ya ibada za wafu hazikubaliwi na Mungu. Na hili jambo la kunyoa upaa kwa ajili ya wafu kumbe linafanywa na jamii nyingi mbalimbali. Na wengine wamejaribu kuliboresha kulingana na hali ya sasa ya ustaarabu duniani; kwa nfano, mfiwa *{wafiwa}* baada ya kunyolewa kidogo sehemu fulani fulani na wale wahusika wa kimila, anakwenda tena kwa

vinyozi wa kitaalamu *{maarufu kwa jina la saluni}* kusawazisha ili kwamba asionekane na kila mtu kwamba amenyolewa kwa ajili ya mfu. Maana huenda yeye ni mkristo muumini wa kawaida ama ni kiongozi kanisani. Lakini utambue kwamba juhudi zo zote zile za kufanya ibada hizi ziwe za kisasa hazisaidii kitu, maana pamoja na hayo yote, bado ibada ni ile ile tu!

Watu wengi kwa maswala ya vifo humuweka Mungu kando kwanza, na baada ya kumaliza ibada hizo potofu wanazozikana wakiwa kanisani ama mbele za watu, ndipo humrudia Mungu. Na mtu wa namna hiyo hastahili kujiita Mkristo; maana anavunja amri ya tatu ya Mungu kwa kulitaja bure jina la Bwana. ***Soma Kutoka 20:7*** Na moja ya makabila yasiyoongoka kwa asilimia kubwa japo si wote kwa swala hili ni Waluo; maana hapa hapategemei cheo chake kanisani wala kwamba ana muda gani tangu ajiite Mkristo. *{Tafadhalini, mniwie radhi niliseme jambo hili kwa ajasiri kwa ajili ya faida/manufaa ya wengi}* Tena Waluo hawa wana jambo la kushangaza; ikiwa wewe ni mkristo wa hivi hivi, kwa maana kwamba unashiriki ibada hizo; au ikiwa wewe ni mpagani halisi mwenye kushiriki ibada hizo, halafu upuuzie usitimize masharti ipasavyo; basi wewe umekwisha! Umekwisha kwa namna gani? Wana ugonjwa wa ajabu *{wa kishirikina/kiimani}* uletwao na yule Shetani ajigeuzaye uitwao **"CHIRA".** Ni ugonjwa usiotibika kitaalamu hospitalini wala kwa dawa za kawaida za miti shamba. Tena ugonjwa huo hukufanya uharishe na kukonda na kuwa sawa na mgonjwa wa UKIMWI; maana hata nywele zako zitateleza na kunyonyoka na mabega kuchonga juu, ni hatari sana! Na kama ni baba au mama hakuzingatia vigezo na masharti; basi familia yote itapitia hali hiyo mbaya ya ugonjwa mmoja baada ya mwingine mpaka wote mfe kabisa. Vinginevyo; watoto watoe kafara kwa hao wafu ndipo wanusurike! Na hii imewafanya watu kuogopa kiasi kwamba japo wanajiita Wakristo; yaani wamfuatao Kristo, lakini hapa wanasema***; "Kristo ngoja kwanza; fanya kuendelea mbele kidogo, tutakutana baadaye".*** Lakini Mungu ashukuriwe; maana wapo Waluo wengi waliojitoa kikamilifu kwa Mungu na wala hawashiriki ibada hizo wala kudhurika na hiyo **"chira".** Tangu leo Mungu anawahitaji majasiri kama hao wamfuate kikamilifu japo kuwa kuna hatari ya kutengwa na jamii zao. Maandiko ya Mungu yanasema; ***"Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli" Yohana 4"23-24.***

Huenda ukajiuliza kwamba; mbona mafungu *{maandiko}* hayo tuliyoyasoma yanawahusu Waisraeli na yana uhusiano gani na sisi wa mataifa mengine? Naam; kumbuka mwanzoni tuliona kuwa ni Mungu ndiye aliyewaumba wanadamu. Na ni kweli kwamba ilifika wakati Mungu alinena na Waisraeli tu kwa makusudi maalumu; maana imeandikwa, ***"…Mungu aliye hai, aliyeumba mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo; ambaye zamani zilizopita aliwaacha mataifa yote waende katika njia zao wenyewe" Matendo 14:15-16.*** Sasa je! vipi kwetu sisi leo hii anatuambiaje? Wapendwa wetu; leo hii Mungu anatuambia, "…***zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni;bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu." Matendo 17:30*** Watu hao ni mimi na wewe tusio Waisraeli wa kimwili. Sasa je! vipi wewe kwa upande wako, utatii agizo la Muumba wako ama utakaidi? **Mwenye masikio na asikie; ni Biblia yasema.**

## Mila na desturi potofu

Mambo hayo tuliyoyaona yahusuyo ibada za wafu ni mila na desturi potofu za kipagani *{kishetani}*. Na hii ni pamoja na misemo potofu itumikayo na wengi kama vile wasemavyo eti; **"Mungu aiweke au ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, amina".** Pamoja na ule usemi mwingine kwamba; **"Sisi tulimpenda marehemu, lakini Mungu amempenda zaidi".** Hii misemo miwili ni maarufu sana; lakini tukuambie tu kwamba misemo hii na mingine kama hii ni misemo

potofu isiyokuwa na ukweli wo wote wa kimaandiko; maana Mungu hana mahali pa kulaza na kuweka roho za waliokufa *{marehemu}.* Tena si kweli kwamba wale wanaokufa ni wale waliopendwa zaidi na Mungu. Hebu jiulize; ikiwa wamependwa zaidi na Mungu na wanakwenda kustarehe pamoja naye; sasa ni kwa nini tunawalilia na kusononeka pale Mungu anapowachukuwa wale awapendao? Na je! sisi tulio hai sasa, ndio kusema kwamba hatupendwi na Mungu; au kwamba anatupenda lakini kidogo tu? Jiadharini na misemo hii, maana ni misemo ya kipagani, japo utaona au kusikia ikitumiwa sana hasa na wale wanaoitwa Wakristo, tena hasa viongozi wa kidini wakati wa misiba na katika maziko.

Na ikiwa sisi tunajiita kuwa ni wafuasi wa Kristo na huku tukiendelea kukumbatia mila na desturi za kishetani; je! sisi ni wafuasi wa huyo Kristo kweli kama tunavyojiita? Hebu yeye Kristo mwenyewe atujibu. Kristo Yesu anasema hivi; ***"Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamuruyo." Yohana 15:14*** Tena anasema; ***"Mkinipenda, mtazishika amri zangu." Yohana 14:15*** Na kumbuka tuliona kwamba tumeamriwa kutofanya ibada za wafu maana ni mila na desturi potofu. Na hii ni kwa mila na desturi zo zote zile hata kama sio zihusuzo wafu tu. Na endapo tunaendelea kushikamana nazo na huku pia tukijiita Wakristo, basi tunajidanganya wenyewe. Maana tukiendelea katika hali hiyo Kristo anatuambia kwamba; ***"Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu." Mathayo 15:8-9.*** Sasa je! mpendwa; utaendelea na mila na desturi za kwenu zilizo za Kishetani ama tangu leo utafuata maagizo ya Mungu muumba wako? Uamuzi ni wako. **Mwenye masikio na asikie; ni Biblia yasema.**

## Sura ya tatu

# KIYAMA YA WAFU {UFUFUO}

Kumekuwa na mabishano makali sana tangu zamani hadi leo juu ya swala la kiyama ya wafu, yaani kuhusu ufufuo wa wafu. Kundi moja linadai kuwa kuna kiyama ya wafu; na kundi lingine linadai kuwa hakuna kiyama ya wafu, kwamba mwisho wa mambo yote ni pale tu mtu anapokufa. Na haya makundi yalikuwepo hata wakati wa Yesu. Mafarisayo waliamini kuwa kuna kiyama ya wafu, huku Masadukayo wao hawakuliamini hilo. ***Soma Mathayo 22:23-33.*** Hali kadhalika leo madhehebu mengi yanaamini kutakuwa na kiyama ya wafu, na huku mengine mengi pia yanakataa habari ya kiyama ya wafu. Sura hii ya kitabu hiki kupitia Biblia takatifu *{yaani, sauti ya Mungu}* itatuamulia swala hili kama kuna kiyama *{yaani, ufufuo}* ama kama haipo kabisa. Sasa basi; kaa makini katika kusoma biblia yako na umwamini Mungu kupitia neno lake, yaani biblia,kwamba kile asemacho Mungu ndicho cha kweli.

Watakatifu wa Mungu tangu agano la kale wamekuwa wakielewa na kuamini juu ya kiyama ya wafu. Na hii ndiyo maana katika kitabu cha Danieli biblia inasema; ***"Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele." Danieli 12:2*** Tena; ***"Lakini enenda zako hata utakapokuwa mwisho ule, maana wewe utastarehe****{utakufa}*, ***nawe utasimama*** *{utafufuka}* ***katika kura yako mwisho wa siku hizo." Danieli 12:13*** Na Ayubu mtumishi wa Mungu pia anasema kwamba; ***"Lakini mimi najua ya kuwa Mteteaji wangu yu hai, Na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi*** *{yaani baada ya kufa}*, ***Lakini, pasipo kuwa na mwili wangu*** *{yaani baada ya kufufuka katika mwili wa roho}* ***nitamwona Mungu; Nami nitamwona mimi nafsi yangu, na***

***macho yangu yatamtazama, wala si mwingine…" Ayubu 19:25-27*** Na kupitia kwa nabii Hosea Mungu anasema***; "Nitawakomboa na nguvu za kaburi;nitawaokoa na mauti;ewe mauti ya wapi mapigo yako? ewe kaburi, ku wapi kuharibu kwako? kujuta kutafichwa na macho yangu". Hosea 13:14*** Maandiko haya pamoja na mengine mengi katika agano la kale yanathibitisha kuwa agano hilo linatambua kiyama ya wafu; maana tumewaona Danieli, Ayubu na Hosea wakifa na matumaini ya kusimama *{kufufuka}* siku ya mwisho.

Na sasa twende katika agano jipya. Katika injili ya Yohana Yesu anatuambia maneno haya kwamba; ***"Msistaajabie maneno hayo;kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu".Yohana 5:28-29*** Naye mtume Paulo pia kwa upande wake anasema kwamba; ***"Nina tumaini kwa Mungu,ambalo hata hao nao wanalitazamia, ya kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia". Matendo 24:15*** Kwa hivyo basi; swala la kufufuka kwa mwanadamu ye yote yule ni la lazima; kwamba ni mwema ama ni mwovu. Maana biblia kama tulivyoona tangu agano la kale mpaka agano jipya pia; imetuthibitishia kwamba kutakuwa na kiyama *{ufufuo}* ya wafu. Tofauti ni malipo ya kila mtu baada ya kufufuliwa kulingana na kazi yake ilivyo. Kitabu cha Wakorintho kinatuambia hivi; ***"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya". 2 Wakorintho 5:10*** Pia katika ufunuo Yesu anasema***; "Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo". Ufunuo 22:12*** Kwa hivyo wapendwa; hakuna haja ya mabishano tena ikiwa tunayaamini Maandiko Matakatifu *{yaani, Biblia}* kuwa ni sauti ya Mungu; maana yanathibitisha kuwa kutakuwa na kiyama*{ufufuo}* ya wafu. ***Wakusikia na asikie; ni biblia yasema.***

## Vipindi tofauti vya ufufuo

Pamoja na madhehebu mengi kuamini juu ya kiyama ama ufufuo wa wafu; lakini wameshindwa kuuelewa ukweli wote kuhusu ufufuo huo. Maandiko tuliyoyasoma hapo nyuma yamelizungumzia swala la ufufuo kwa ujumla wake. Na kwa kutokujua jinsi ya kujifunza na kuielewa biblia; basi maandiko hayo yamewafanya wao kujua kwamba kutakuwa na siku moja tu ya ufufuo *{Na ili kujua jinsi ya kujifunza na kuielewa biblia kwa usahihi; basi agiza ujumbe wetu usemao,* ***"WAPI PA KUANZIA",*** *ili ujifunze zaidi, na tutakutumia bure ujumbe huo}.* Hata hivyo; ni **KANISA LA MUNGU** pekee ndilo linaloutambua ukweli wote wa jambo hili; maana imeandikwa; ***"Wakaja wanafunzi, wakamwambia, Kwa nini wasema nao kwa mifano? Akajibu, akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni,bali wao hawakujaliwa". Mathayo 13:10-11*** Basi kwa kuwa hawakujaliwa, maandiko hayo yamekuwa kwao kama mifano. Na hili swala tunalolizungumzia hapa hivi sasa, ni moja ya hizo siri za ufalme wa mbinguni. Na hivyo basi; kwako wewe kufikiwa na ujumbe huu wa siri ya Mungu, ni neema *{bahati}* ya ajabu kwako usiyopaswa kuipuuza.

Tayari tumekwishatambua kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu kwa walio wema na kwa waovu pia. Lakini huo ufufuo utakuwa na vipindi tofauti tofauti kama Mungu mwenyewe alivyopanga. **Ufufuo umegawanyika katika vipindi vikuu vitatu; kwa maana kwamba kutakuwa na ufufuo wa kwanza, ufufuo wa pili na ufufuo wa tatu.** Huenda kufikia hapa pengine wengi wenu mkaanza kushangaa sana. Lakini kama tulivyotangulia kusema; hii ni moja ya siri za Mungu; hivyo basi kaa makini katika kuyachunguza maandiko kama watu wa Beroya. ***"Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo". Matendo 17:11*** Hivyo basi ili uielewe hii siri ya Mungu; sio ushangae na kuachana nayo; bali uyachunguze

maandiko kwa makini, na kwa kuomba uongozi wa roho mtakatifu wa Mungu ili akuwezeshe kuona ikiwa kwamba jambo hili ndivyo lilivyo ama sivyo. Fuatana nasi tafadhali.

## Ufufuo wa kwanza

Kule kuja kwa Yesu Kristo tunakokutazamia sasa ndiko kutakaoleta huu ufufuo wa kwanza. Na huu ufufuo ni kwa ajili ya watakatifu wa Mungu tu; wale ambao wameushinda ulimwengu wa dhambi pamoja na anasa zake zote, na sasa wanafanywa wana kamili wa Mungu. Wanazaliwa mara ya pili katika miili ya roho na hawawezi kutenda dhambi tena. ***"Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu". 1 Yohana 3:9*** Mtume Paulo anatuambia kwamba; ***"Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu;nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani;na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele".1 Wathesalonike 4:13-17*** Je! wapendwa; mmesikia kwamba waovu pia watafufuliwa wakati huo? Ni wale tu waliokufa katika Kristo ndio watakaofufuliwa wakati huo wa kuja kwa Yesu. Soma pia ***1 Wakorintho 15:42-54***. Hawa watakatifu wakiisha kufufuliwa na kuungana na watakatifu watakaokuwa hai wakati ule; wakiishakubadilishwa na kupewa miili ya roho na kuwa kama Mungu alivyo; basi Mungu atawapa kuitawala Dunia hii kwa miaka elfu moja pamoja na Yesu. Wakati huo waovu watakuwa hawajafufuliwa bado.

Mtume Yohana anasema kwamba; ***"Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu;nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao;nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu. Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu. Huu ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu;bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu". Ufunuo 20:4-6***

Maandiko yanasema kwamba; baada ya kufufuliwa kwa hawa watakatifu wa Mungu; basi hao wafu waliosalia hawakuwa hai hata itimie ile mika elfu. Na hii ni kwa sababu; kuja kwa Yesu kule tunakokutazamia hivi sasa, ni kwa ajili ya kuurejesha tena ufalme wa Mungu hapa duniani; ufalme ambao utatawaliwa na hao watakatifu wake {Kwa maelezo ya kina zaidi kuhusu fundisho hili; basi agiza kitabu chetu kisemacho ***"UFALME WA MBINGUNI***", ili ujifunze zaidi, na tutakutumia bure}. Basi kitabu cha ufunuo kinaendelea kufafanua wazi kikisema; ***"Nao waimba wimbo mpya wakisema;Wastahili wewe*** *{Yesu}* ***kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake;kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu;nao wanamiliki juu ya nchi". Ufunuo 5:9-10*** Wapendwa; kuja kwa Yesu Kristo tunakokungojea hivi sasa ndiko anakokuzungumzia nabii Danieli akisema; ***"Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake;bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele". Danieli 2:44*** Tena Danieli anazidi kusema kwamba, baada ya ujio huo wa kristo, na baada ya kuwa amewafufua

watakatifu wake na kuwafanya kuwa viumbe wa kiroho***;*** basi kuanzia hapo ndipo ***"… ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote*** *{sio juu mbinguni},* ***watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele, na wote wenye mamlaka watamtumikia*** *{Yesu}* ***na kumtii". Danieli 7:27*** Na kwa sababu hiyo basi; huu ufufuo wa kwanza ni kwa wale tu wanaozijua na kuzitenda siri za Mungu. Na kwa kuwa wataitawala dunia yote; wao watakatifu wa zamani kwa kupitia roho mtakatifu pamoja na watakatifu wa sasa kwa kupitia roho yule yule mtakatifu {ambaye pia ni maandiko ya Mungu}; walipewa na wanapewa semina ya utawala wa ufalme wa mbinguni. Na kwa kuwa watakuwa makuhani *{yaani, waalimu wa neno la Mungu}*,basi wamepewa siri zote za Mungu ambazo watazifundisha watu wote kwa muda wa hiyo miaka elfu moja. Mtu ye yote yule asiyejua na kutembea katika hizi siri za Mungu, hawezi kufufuka katika huu ufufuo wa kwanza; maana hata yeye mwenyewe halifahamu jambo hili. Pamoja na wewe kujiita Mkristo ama mcha Mungu; lakini kama Mungu hakukujalia kuzijua siri zake hizi, na hivyo kwamba huenendi sawasawa na neno hili {soma Isaya 8:20}, basi huwezi kufufuka katika huu ufufuo wa kwanza. Maana ikiwa wewe mwenyewe hujui lo lote kuhusu hizi siri za Mungu na mipango yake; utawezaje basi kuwa kuhani *{mwalimu}* wa Mungu na kuwafundisha watu kile usichokijua wewe?

Wapendwa; **Huu ndio ufufuo wa kwanza**. Heri na mtakatifu ni yeye aliye na sehemu katika huu ufufuo; maana wao mara tu baada ya ujio wa Yesu Kristo, watapewa miili ya roho isiyoweza kufa; nao watafanana na Yesu mwenyewe huku wakitawala pamoja naye milele. ***Soma 1 Yohana 3:1-3***

## Ufufuo wa pili

Biblia inatuambia katika ***Yohana 3:16*** kwamba***; "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu,hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee,bali awe na uzima wa milele".*** Na tena inasema; ***"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote,kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo". Matendo 4:12*** Tumeona jinsi ambavyo ufufuo wa kwanza unahusika na watakatifu pekee; tena ambao ni wachache ukilinganisha na idadi ya wanadamu wote duniani. Na makusudi ya Mungu ni kwamba kila mtu aokolewe pasipo kubagua kabila, lugha, jamaa wala taifa lake; maana biblia imesema ***"Mungu aliupenda ulimwengu".*** Na zaidi ya yote; ni jina moja tu walilopewa wanadamu kwa ajili ya wokovu, yaani jina la Yesu Kristo.

Sasa je! ni nini hatima ya wale waliokufa na wanaoendelea kufa pasipo kusikia hilo jina la Yesu wala habari zake? Kwa mfano mwepesi; hebu jaribu kufikiria juu ya babu zako waliokufa kabla ya wamishonari kuja na kufundisha *{kuhubiri}* kuhusu huyo Yesu; unadhani Mungu atawaweka katika kundi gani; la wema ama la waovu? Waliokufa na wanaoendelea kufa pasipo kushuhudiwa ukweli kuhusu Yesu japokuwa ni wenye dhambi, kamwe Mungu hawezi kuwahukumia adhabu maana anasema asiyeliamini hilo jina la Yesu ndiye atakaye hukumiwa. ***Soma Marko 16:16.*** Na vile vile Mungu hawezi kuwahesabia haki *{kuwaita wema}* na huku ni wenye dhambi. ***Soma Kutoka 34:7.*** Hali kadhalika wale wote ambao pia hawajafikiwa na injili ya kweli ya Yesu Kristo *{yaani, mafundisho ya kweli ya biblia na si mahubiri na mafundisho ya mapokeo ya kimadhehebu ya kidini}* inayohubiriwa na Kanisa la Mungu; na hivyo kwamba wakifa kabla ya ujio wa Yesu; basi hao nao Mungu anawahesabu kwamba hawajalisikia jina la Yesu; maana kile walichohubiriwa na kukisikia sicho kile ambacho Mungu amekikusudia wakisikie. Na watu hawa wote kwa pamoja ndio waliopangiwa ufufuo wa pili. Hapa ndipo utabiri wa nabii Ezekieli katika sura ya 37 ya kitabu chake utakapotimia. Katika unabii huo watu wote hawa wamefananishwa na mifupa mikavu. Na hii itakuwa ni baada ya ile miaka elfu moja ya utawala wa Yesu na Watakatifu wake kutimia. Mungu alizungumza na Ezekieli akisema; ***"…Mwanadamu, Je mifupa hii yaweza kuishi?"*** Naye Ezekieli

akajibu; ***"Ee Bwana Mungu, wajua wewe."*** Kisha Mungu akamwambia tena; ***"Toa unabii juu ya mifupa hii, uiambie, Enyi mifupa mikavu, lisikieni neno la Bwana. Bwana Mungu aiambia mifupa hii maneno haya; Tazama, nitatia pumzi ndani yenu, nanyi mtaishi. Nami nitatia mishipa juu yenu, nami nitaleta nyama iwe juu yenu, na kuwafunika ngozi, na kutia pumzi ndani yenu, nanyi mtaishi;nanyi mtajua ya kuwa mimi ndimi Bwana". Ezekieli 37:3-6*** Na kwa kuyafafanua maono haya Mungu anamwambia Ezekieli kwamba; ***"Basi tabiri, uwaambie, Bwana Mungu asema hivi; Tazama, nitafunua makaburi yenu, na kuwapandisha kutoka katika makaburi yenu, enyi watu wangu, nami nitawaingizeni katika nchi ya Israeli. Nanyi mtajua ya kuwa mimi ndimi Bwana, nitakapoyafunua makaburi yenu, na kuwatoa ninyi katika makaburi yenu, enyi watu wangu. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, nanyi mtaishi, nami nitawawekeni katika nchi yenu, nanyi mtajua ya kuwa mimi, Bwana, nimesema hayo, na kuyatimiza, asema Bwana" Ezekieli 37:12-14.***

Baada ya watu hawa kufufuliwa, biblia inasema watapewa roho mtakatifu kwa wingi na kuwaondolea mioyo migumu, ili waweze kuelewa na kuyashika maagizo *{sheria}* ya Mungu ambayo watafundishwa na wale makuhani wa Mungu *{yaani watakatifu}*, ***Soma Ezekieli 36:25-27***. Watu hawa watashuhudia amani itakayoletwa na utawala wa Yesu *{yaani ufalme wa mbinguni}* na watafundishwa ukweli wote kumuhusu Mungu, maisha yake na kusudi lake la uumbaji. Na kama vile maji yajaavyo bahari, ndivyo kumjua Mungu kutakavyojaa katika mioyo ya watu wote ***{Soma Isaya 11:6-9 Habakuki 2:14}.*** Ni kipindi hiki pamoja na watu hawa ndio ambao Yohana anaeleza habari zao akisema; ***"Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake" Ufunuo 20:11-13.***

Naam; baada ya kuwa vitabu vimefunguliwa kwa watu hawa na injili ikahubiriwa kwao; na kila mmoja kupata nafasi ya kuyafahamu makusudi na mapenzi ya Mungu; bado kila mtu atakuwa na uhuru wa kuchagua maisha ayatakayo mwenyewe, kwamba ni njia ya Mungu ya uzima ama ni njia ya Shetani ya mauti. Na ni hakika kwamba watu wengi kwa vile wameonja ladha ya utawala bora wa Mungu, watayapinga maisha yale ya awali ya Shetani ili waendelee kuishi maisha hayo ya raha mustarehe.

Baada ya ufufuo huo wa pili kufanyika; watu wa ufufuo huo watapewa muda wa miaka mia moja kwa ajili ya kujifunza maisha ya Mungu ili baada ya hapo, kila mmoja afanye uamuzi juu ya hatima ya maisha yake, yaani achague kumtii Mungu na hivyo kwamba abadilishwe kuwa kiumbe wa kiroho na kuishi milele; ama kwamba amkaidi Mungu na hivyo kuchagua mauti ya milele. Biblia inaeleza kwamba; ***"Hatakuwapo tena mtoto wa siku chache, wala mzee asiyetimia siku zake; kwa maana mtoto atakufa mwenye umri wa miaka mia; bali mtenda dhambi mwenye umri wa miaka mia atalaaniwa" Isaya 65:20.***

Na hivyo basi; kufikia hapo, watu wote watakuwa wameshuhudiwa na kuhubiriwa injili ambayo ni habari njema ya ufalme wa mbinguni unaoambatana na uzima wa milele. Na kila atakayeamini ataokolewa, na yule asiyeamini atahukumiwa ***{soma Marko 16:16}.*** Na mwisho wa siku hizo mia moja biblia inasema watu hao ***"Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto. Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto" Ufunuo 20:13-15.***

## Ufufuo wa tatu

Wale wote ambao walikufa na wanaoendelea kufa mpaka sasa, na huku wakiijua kweli yote ya biblia na wakashindwa kusimama katika hiyo kweli mpaka mwisho; hawatafufuka katika ufufuo wa kwanza wala katika ufufuo wa pili. Watu hawa ndio watakaohusika na ufufuo wa tatu ambao pia huitwa ufufuo wa hukumu. Je! ni kwanini ufufuo huu unaitwa ufufuo wa hukumu? Hii ni kwa sababu watu hawa hawana udhuru *{sababu ya kujitetea}* tena mbele za Mungu; maana tayari Mungu wanamjua, na neno lake *{yaani maandiko}* pia wanalijua *{kwa maana kwamba; wanayajua matakwa ya Mungu kwao},* isipokuwa tu hawakuzingatia na kushikamana mpaka mwisho na lile walijualo {***Soma Mathayo 7:24-27  Marko 16:15-16}***. Maana biblia inasema; ***"Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo, wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehesha kwa dhamiri" Waebrania 6:4-6.***

***"Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi;bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao. Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu. Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?" Waebrania 10:26-29.*** Basi wapendwa; hii ina maana kwamba, kila mtu amepewa nafasi moja tu ya wokovu. Na hivyo basi; ikiwa umepewa neema ya kuitwa sasa katika Kanisa hili la Mungu na ukaipuuza; basi tambua kwamba, hauna nafasi nyingine tena ya kuokolewa. Sasa je! utajuaje kuwa Mungu amekuita katika Kanisa lake? Ni rahisi sana. Ujumbe huu unaousoma hivi sasa ni sauti ya Mungu kwako. Tafadhali basi usiupuuze. Kumbuka, heri na mtakatifu ni yeye aliye na sehemu katika ule ufufuo wa kwanza. Kadhalika na wale wa ufufuo wa pili; endapo mtu ataipuuza neema hiyo waliyopewa; basi hatakuwa na nafasi nyingine tena ya kuokolewa. Ufufuo wa tatu ni kwa ajili ya wale waliokwisha kuijua kweli yote na wasiitende hiyo kweli, na hivyo kwamba wanafufuliwa kwa ajili ya hukumu, yaani mauti ya milele.

Wapendwa; hivi ndivyo mambo yalivyo kuhusu kifo na kiyama ya wafu kwa mujibu wa Maandiko Matakatifu ya Mungu. Wala usidanganyike tena tangu sasa na mafundisho ya uongo na mapokeo ya wanadamu; kwamba ni wapagani au kwamba wanajiita wakristo. Naam; ***"…ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi" Isaya 8:20;*** usiwasikilize kabisa. Maana wao wanafundisha kila mmoja imani yake na sio ukweli halisi wa biblia maana hawaijui hiyo kweli. ***Soma Yohana 8:44  2 Timotheo 3:5,7-***8. Wakusikia na asikie.

## Sura ya nne

# NI NINI HATIMA YA WOTE WANAOKATAA KUTUBU?

Japokuwa Mungu atatoa nafasi kubwa sana ya wokovu kwa wote ambao hawakumjua, lakini baadhi yao watakataa kutubu, wala kujinyenyekeza kwa Mungu ili wapokee zawadi yake ya uzima wa milele. Sasa basi; ni nini hatima ya watu hao? Biblia inafunua wazi kwamba, watu hao hawataendelea kuishi huku wakiteseka kwa kuungua ndani ya moto milele kama ambavyo watu wengi wanavyofundisha; bali wataangamizwa kabisa na kuwa kana kwamba hawakuwahi kuwepo kabisa! Ufunuo 20:15 inatuambia kuwa, baada ya hukumu ya mwisho ya awamu ya tatu ya wokovu, ***"iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto"*** Na tena inaongeza kusema; ***"Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili" Ufunuo 21:8.***

Ieleweke hapa vizuri, kwamba hatima *{mwisho}* ya wote wanaokataa kutubu ni mauti ya milele na wala si kuendelea kuishi ndani ya moto huo milele kwa maumivu mengi! Mtume Paulo pia alifahamu kuwa mwisho wa waovu wote ni mauti ya milele, na akasema; ***"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" Warumi 6:23.*** Hapa anabainisha wazi kwamba kuendelea kung'ang'ania dhambi zetu, mwisho wake ni mauti ya milele; na kukubali kutakaswa na kafara ya Kristo iliyotolewa kwa ajili yetu, mwisho wake ni uzima wa milele.

Naye nabii Malaki anaweka wazi hatima ya waovu wote akisema; ***"Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema BWANA wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi. Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kuchezacheza kama ndama wa mazizini. Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema BWANA wa majeshi" Malaki 4:1-3.***

Wapendwa; Mungu wetu ni mwenye upendo na rehema nyingi sana, na kamwe hapendi kuwatesa wanadamu wala kuwaua ***{soma Maombolezo 3:33; Ezekieli 18:23,30-32}***; na hivyo basi hawezi kuvumilia kuwaona wanadamu aliowaumba kwa mfano wake *{japokuwa wamemkataa}* wakiendelea kuteseka ndani ya moto kwa maumivu ya milele! Na badala yake, moto utawateketeza mara moja, na kugeuka makapi na majivu, wasiwepo tena kabisa milele. Mungu wetu ni Mungu mwenye huruma na rehema ajabu!

Mafundisho ya kwamba waovu watateswa milele na milele katika moto wa Jehanamu ni mafundisho ya uongo na mapokeo ya wanadamu na msingi wake ni Shetani mwenyewe ambaye ni baba wa uongo ***{soma Yohana 8:44};*** wala si mafundisho ya kweli ya biblia. Na tutambue kwamba; kuendelea kuamini katika ibada za mapokeo na mafundisho ya wanadamu ni machukizo kwa Mungu, maana Mungu mwenyewe anasema; ***"Watu hawa huniheshimu kwa midomo Ila mioyo yao iko mbali nami; Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu. Ninyi mwaiacha amri*** *{mafundisho}* ***ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu" Marko 7:6-8.*** Wapendwa; mwenye masikio na asikie!

## Je! kulia unapofiwa ni dhambi?

Kumetokea watu wengi siku hizi wanaojiita waalimu na wachungaji ambao wamewazuia waumini wao kulia pale wanapofiwa na wapendwa wao. Kibaya zaidi ni kule kusingizia kwamba ni biblia ndiyo iliyokataza. Tangu mwanzo biblia imeonesha sehemu kadha wa kadha wacha Mungu wakiwalilia na kuwaomboleza wapendwa wao wanaokufa. Kwa mfano; tukiangalia katika kitabu cha Mwanzo tunawaona wana wa Yakobo *{Waisraeli}* wakimlilia baba yao na kumuomboleza***. "Wakaja mpaka sakafu ya Atadi, iliyo ng'ambo ya Yordani. Wakaomboleza huko maombolezo makuu, mazito sana. Akafanya*** *{Yusufu}* ***matanga ya babaye siku saba" Mwanzo 50:10.*** Vile vile hata nabii Musa alipokufa,Waisraeli wakamlilia na kumwomboleza. ***"Wana wa Israeli wakamwomboleza Musa katika uwanda wa Moabu siku thelathini;basi siku za maombolezo ya matanga ya Musa zikaisha" Torati 34:8.*** Biblia haijamzuia mtu awaye yote kulia pale anapofiwa,wala haijazuia maombolezo wala kufanya matanga.

Kwa nini tunalia pale tunapofiwa? Ni kwa sababu ya uchungu wa kuachwa *{kutokwa}* na wapendwa wetu ambao tulizoeana nao na kushirikiana nao katika mambo mbalimbali, ambao sasa mauti inatutenganisha nao tusiweze kuwaona tena kwa sasa. Na hata Bwana wetu Yesu pia alihudhuria katika misiba ya vifo alipokuwa hapa duniani {***Soma Mathayo 9:23-26}***. Wakati rafiki yake wa karibu sana Lazaro alipokufa,Yesu hakujizuia kulia machozi***. "Yesu akalia machozi. Basi Wayahudi wakasema, Angalieni jinsi alivyompenda" Yohana 11:35-36.*** Lakini ipo tofauti kubwa sana kati ya wacha Mungu wa kweli ukilinganisha na watu wengine. Na tofauti iliyopo kati yao ni hii kwamba; Wacha Mungu wanalia kwa sababu ya uchungu unaowashika ghafla, na baada ya maombolezo ya muda mfupi pamoja na matanga kufanyika; basi wao hawana haja ya kuendelea kulia na kuomboleza tena zaidi. Na hii ni kwa sababu wanayo matumaini ya kuwaona tena wapendwa wao waliofikwa na mauti, maana wanaamini juu ya ufufuo wa wafu**.** Wanaamini na kufarijika katika maandiko mengi ikiwa ni pamoja na haya yasemayo kwamba; ***"Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye...Basi farijianeni kwa maneno hayo" 1 Wathesalonike 4:13-14,18.*** Na kwa mcha Mungu; ikiwa mtu kwa uwezo wa roho mtakatifu amepewa uwezo wa kustahimili ama kuvumilia uchungu *{kujizuia kulia}* wa mauti na hivyo kwamba asiwe na sababu ya kulia; basi hiyo si dhambi kwake na ni sawa tu na wala mtu ye yote asimsumbue, bali ikiwezekana ajifunze kwake, maana mtu huyo imani yake ni kubwa na imara siyoweza kutikiswa na nguvu za mauti.

Wale wasiomcha Mungu, wao wanalia pasipo matumaini, kwani wao wanaamini kuwa hawataonana tena milele; kinyume kabisa na wacha Mungu ambao biblia inatuambia tusije tukahuzunika kama hao wasio na matumaini. Kile kinachoshangaza; utasikia katika sehemu za maziko watu wakisema; Mungu aiweke ama ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi; maana wao wanaamini kwamba huko peponi ndiko anakoishi Mungu pamoja na wale waliokufa na ni katika maisha ya raha mustarehe. Na huenda huyo marehemu kabla ya kufa kwake alikuwa akiteseka kwa maumivu makali ya magonjwa kwa muda mrefu hapa duniani. Sasa je! ikiwa baada ya kufa, mtu huyo anahamia peponi kwenye maisha ya raha mustarehe pamoja na Mungu; ninyi mnalilia nini? Je! mnataka arudishwe tena katika dhiki na shida zilizokuwa zimemchosha? Sasa basi; uko wapi upendo wenu ikiwa mnamwonea wivu marehemu mpaka mnalia kwa vile yeye amepata maisha mema? Wapendwa wetu; badilikeni tangu sasa, maana Mungu anawaita mtoke katika upotofu huo.

Kwa hivyo tusemalo ni kwamba; biblia haimzuii mtu kulia anapofiwa na wala haimuamuru *{haimlazimishi}* mtu kulia anapofiwa; yaani wewe ulie ama usilie ni juu yako na wala si dhambi. Na kama si wewe uliyefiwa bali ni jirani, rafiki ama Mkristo mwenzako; basi biblia inatuambia kwamba***;***

***"Kwa pendo la undugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu…Furahini pamoja nao wafurahio; lieni pamoja nao waliao" Warumi 12:10,15.*** Tena inatuambia; ***"Heri kuiendea nyumba ya matanga, Kuliko kuiendea nyumba ya karamu. Kwa maana huo ndio mwisho wa wanadamu wote, naye aliye hai atautia moyoni mwake" Mhubiri 7:2.*** Je! unadhani ni kwa nini Mhubiri anasema kwamba aliye hai anapaswa kufikiria juu ya siku ya kufa kwake? Jibu ni hili; ***"Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa, lakini wafu hawajui neno lo lote..." Mhubiri 9:5.*** Sasa basi; ikiwa wafu hawajui neno lo lote, na huku sisi tulio hai tunajua kwamba tutakufa; je! hii inatuambia kwamba kuna kitu muhumu sana tunapaswa kufanya katika siku za uhai wetu? Jibu ni Ndiyo**.** Maana; ***"Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu" Mhubiri 12:13;*** soma pia ***Isaya 55:6-7.*** Basi tunapowaona wenzetu wakifa; kwamba wameugua kwa muda mrefu ama kwamba wamekufa ghafla; basi hiyo iwe ni changamoto kwetu maana tujiulize; vipi kama sisi tukifa sasa hivi, je! tunautarajia ufufuo wa kwanza ulio kwa ajili ya watakatifu tu huku tukiulinganisha na mwenendo wa maisha yetu ya sasa ulivyo? Kumbuka kila mtu anayo nafasi moja tu ya kuokolewa. Hivyo basi ni vema tukijililia nafsi zetu wenyewe kwa ajili ya wokovu wetu.

## Hitimisho

Ndugu msomaji; leo Mungu wa mbinguni amekujulisha moja ya siri zake ndani ya biblia kupitia kitabu hiki. Sasa je,ungependa kuzijua zaidi siri nyingine nyingi za Mungu? Tunavyo vitabu vingi kwa ajili yako kama vile; "**Kufa na Kufufuka kwa Yesu", "Ufalme wa mbinguni", "Pasaka", "Jamii ya Mungu", "Kuzaliwa mara ya pili", "Kuokoka na Kuongoka", "Amri kumi", "Siku kuu za Mungu", "Dini za mitindo",** pamoja na vingine vingi vinavyoeleza ukweli wa biblia pekee na si mafundisho ya madhehebu ama mawazo ya watu fulani tu. Pia ukiwa na swali lolote kuhusu biblia tuulize, na biblia hiyo ndiyo itakayokujibu. Kumbuka kwamba vitabu hivi vyote vinatolewa bure kwako, haviuzwi. Cha kufanya wewe wasiliana nasi kwa anuani zifuatazo;

**KANISA LA MUNGU – TANZANIA**

**Idara ya uandishi na usambazaji - MWANZA**
Simu: +255 753 359 179, +255 688 359 179 & +255 655 659 179.
Barua pepe; Ukweliwabiblia@yahoo.com.sg

**Idara ya usambazaji:**
MARA – Simu: +255 755 409 202
ARUSHA – Simu: +255 754 028 574, +255 782 422 216.
DAR ES SALAAM – Simu: +255 762 055 056, +255 672 611 204.

**KANISA LA MUNGU – KENYA**
Barua pepe: endcog@gmail.com